

**KUMB: PPR/2020 - 02/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI  
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 5 FEBRUARI 2020**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 5 Februari 2020**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa nchini kupitia **bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Januari 2020. Kwa mwezi Februari 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 20/lita (sawa na asilimia 0.96), Shilingi 74/lita (sawa na asilimia 3.51) na Shilingi 44/lita (sawa na asilimia 2.13), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 20.01/lita (sawa na asilimia 0.96), Shilingi 74.21/lita (sawa na asilimia 3.72) na Shilingi 43.96/lita (sawa na asilimia 2.25), mtawalia.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika mkoa wa Tanga zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Januari 2020. Kwa mwezi Februari 2020, bei za rejareja za Petroli na Mafuta ya Taa kwa **Mikoa ya Kaskazini** (yaani Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara) zimeongezeka kwa Shilingi 42/lita (sawa na asilimia 1.95) na Shilingi 2/lita (sawa na asilimia 0.11), mtawalia wakati bei za mafuta ya Dizeli zimepungua kwa Shilingi 18/lita (sawa na asilimia 0.82), Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 41.94/lita (sawa na asilimia 2.06) na Shilingi 2.37/lita (sawa na asilimia 0.12), mtawalia wakati bei za mafuta ya Dizeli zimepungua kwa Shilingi 17.49/lita (sawa na asilimia 0.87).
- (c) Vilevile, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Mtwara zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Januari 2020. Kwa mwezi Februari 2020, bei za rejareja za mafuta ya Petroli katika **Mikoa ya Kusini (yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma)** zimeongezeka kwa Shilingi 35/lita (sawa na asilimia 1.62) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 22/lita (sawa na asilimia 0.99). Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimeongezeka kwa Shilingi 35.27/lita (sawa na asilimia 1.71) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 21.49/lita (sawa na asilimia 1.05). *Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.*
- (d) Mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata

maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

#### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,226</b>	<b>2,195</b>	<b>2,119</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,257</b>	<b>2,180</b>	<b>2,126</b>
Arumeru (Usa River)	2,257	2,180	2,126
Karatu	2,275	2,198	2,144
Longido	2,268	2,191	2,136
Monduli	2,262	2,185	2,131
Monduli-Makuyuni	2,267	2,190	2,136
Ngorongoro (Loliondo)	2,341	2,265	2,210
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>2,231</b>	<b>2,200</b>	<b>2,123</b>
Bagamoyo	2,237	2,206	2,130
Bagamoyo (Miono)	2,268	2,237	2,161
Chalinze Junction	2,240	2,210	2,133
Chalinze (Msata)	2,244	2,214	2,137
Kibiti	2,247	2,216	2,139

Kisarawe	2,233	2,202	2,126
Mkuranga	2,236	2,205	2,129
Rufiji	2,254	2,223	2,146
<b>Dodoma</b>	<b>2,285</b>	<b>2,254</b>	<b>2,178</b>
Bahi	2,292	2,261	2,185
Chamwino	2,280	2,249	2,173
Chemba	2,311	2,281	2,204
Konoda	2,318	2,287	2,210
Kongwa	2,282	2,251	2,175
Mpwapwa	2,286	2,255	2,179
Mtera (Makatopora)	2,304	2,273	2,197
<b>Geita</b>	<b>2,392</b>	<b>2,361</b>	<b>2,284</b>
Bukombe	2,381	2,350	2,273
Chato	2,413	2,382	2,305
Mbogwe	2,430	2,399	2,322
Nyang'hwale	2,407	2,376	2,299
<b>Iringa</b>	<b>2,290</b>	<b>2,259</b>	<b>2,183</b>
Ismani	2,295	2,265	2,188
Kilolo	2,295	2,264	2,187
Mufindi (Mafinga)	2,300	2,270	2,193
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,442</b>	<b>2,411</b>	<b>2,334</b>
Biharamulo	2,416	2,385	2,309
Karagwe (Kayanga)	2,458	2,427	2,351
Kyerwa (Ruberwa)	2,464	2,433	2,357
Muleba	2,442	2,411	2,334
Ngara	2,429	2,399	2,322
Misenyi	2,450	2,419	2,343
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,434</b>	<b>2,403</b>	<b>2,327</b>
Mlele (Inyonga)	2,416	2,385	2,309
Mpimbwe (Majimoto)	2,427	2,396	2,320
Tanganyika (Ikola)	2,452	2,421	2,345
<b>Kigoma</b>	<b>2,458</b>	<b>2,427</b>	<b>2,350</b>
Uvinza (Lugufu)	2,470	2,439	2,363
Buhigwe	2,447	2,416	2,339
Kakonko	2,415	2,384	2,307
Kasulu	2,444	2,413	2,336
Kibondo	2,422	2,391	2,315
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>2,246</b>	<b>2,170</b>	<b>2,115</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,249	2,173	2,118
Mwanga	2,239	2,163	2,108
Rombo (Mkuu)	2,263	2,186	2,132
Same	2,232	2,156	2,101
Siha (Sanya Juu)	2,253	2,176	2,122
<b>Lindi</b>	<b>2,235</b>	<b>2,161</b>	<b>2,178</b>
Lindi-Mtama	2,240	2,165	2,196
Kilwa Masoko	2,259	2,185	2,153
Liwale	2,270	2,196	2,199
Nachingwea	2,255	2,181	2,207
Ruangwa	2,261	2,187	2,209
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,291</b>	<b>2,214</b>	<b>2,160</b>

Hanang (Katesh)	2,301	2,224	2,170
Kiteto (Kibaya)	2,306	2,229	2,175
Mbulu	2,303	2,227	2,172
Simanjiro (Orkasumet)	2,323	2,246	2,192
<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,405</b>	<b>2,374</b>	<b>2,297</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,446	2,415	2,338
Rorya (Ingirijuu)	2,414	2,383	2,306
Rorya (Shirati)	2,448	2,418	2,341
Bunda	2,396	2,365	2,289
Bunda (Kisorya)	2,406	2,375	2,298
Butiama	2,402	2,371	2,294
Serengeti (Mugumu)	2,450	2,420	2,343
Tarime	2,416	2,385	2,309
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,420	2,390	2,313
<b>Mbeya</b>	<b>2,333</b>	<b>2,302</b>	<b>2,226</b>
Chunya	2,343	2,312	2,235
Chunya (Makongolosi)	2,357	2,326	2,250
Kyela	2,349	2,318	2,242
Mbarali (Rujewa)	2,317	2,287	2,210
Rungwe (Tukuyu)	2,342	2,311	2,235
<b>Morogoro</b>	<b>2,251</b>	<b>2,220</b>	<b>2,144</b>
Mikumi	2,267	2,236	2,159
Kilombero (Ifakara)	2,289	2,258	2,182
Kilombero (Mlimba)	2,311	2,281	2,204
Kilombero (Mngeta)	2,301	2,270	2,193
Ulanga (Mahenge)	2,300	2,269	2,192
Malinyi	2,310	2,279	2,203
Kilosa	2,270	2,239	2,162
Gairo	2,270	2,239	2,162
Mvomero (Wami Sokoine)	2,262	2,231	2,154
Mvomero (Sanga Sanga)	2,251	2,220	2,144
Turiani	2,276	2,245	2,169
<b>Mtwara</b>	<b>2,221</b>	<b>2,147</b>	<b>2,191</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,258	2,183	2,240
Masaki	2,237	2,163	2,217
Newala	2,242	2,168	2,223
Tandahimba	2,235	2,161	2,216
Nanyamba	2,235	2,161	2,216
<b>Mwanza</b>	<b>2,376</b>	<b>2,345</b>	<b>2,269</b>
Kwimba	2,394	2,363	2,287
Magu	2,384	2,354	2,277
Misungwi	2,371	2,340	2,263
Sengerema	2,409	2,378	2,301
Ukerewe	2,436	2,405	2,329
<b>Njombe</b>	<b>2,319</b>	<b>2,288</b>	<b>2,211</b>
Njombe (Kidegembye)	2,339	2,308	2,232
Ludewa	2,357	2,326	2,249
Makambako	2,311	2,280	2,204
Makete	2,349	2,319	2,242
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,316	2,286	2,209

<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,399</b>	<b>2,368</b>	<b>2,292</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,399	2,368	2,292
Kalambo (Matai)	2,406	2,376	2,299
Nkasi (Namanyeleye)	2,413	2,382	2,305
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>2,307</b>	<b>2,233</b>	<b>2,242</b>
Mbinga	2,319	2,245	2,276
Namtumbo	2,298	2,224	2,272
Nyasa (Mbamba Bay)	2,345	2,271	2,286
Tunduru	2,272	2,198	2,301
<b>Shinyanga</b>	<b>2,355</b>	<b>2,324</b>	<b>2,248</b>
Kahama	2,369	2,338	2,261
Kishapu	2,384	2,353	2,276
Ushetu (Nyamilangano)	2,386	2,356	2,279
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	<b>2,397</b>	<b>2,366</b>	<b>2,289</b>
Busega (Nyashimo)	2,390	2,359	2,282
Itilima (Lagangabilili)	2,400	2,369	2,292
Maswa	2,388	2,357	2,281
Meatu (Mwanhuzi)	2,395	2,364	2,288
<b>Singida</b>	<b>2,317</b>	<b>2,286</b>	<b>2,210</b>
Iramba	2,329	2,298	2,222
Manyoni	2,301	2,271	2,194
Ikungi	2,312	2,282	2,205
Mkalama (Nduguti)	2,341	2,311	2,234
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,343</b>	<b>2,312</b>	<b>2,235</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,349	2,319	2,242
Ileje	2,346	2,316	2,239
Momba (Chitete)	2,352	2,321	2,244
Tunduma	2,347	2,316	2,239
<b>Tabora</b>	<b>2,380</b>	<b>2,350</b>	<b>2,273</b>
Igunga	2,334	2,304	2,227
Kaliua	2,399	2,369	2,292
Ulyankulu	2,394	2,363	2,286
Nzega	2,345	2,314	2,238
Sikonge	2,392	2,361	2,285
Urambo	2,394	2,363	2,286
Uyui	2,381	2,351	2,274
<b>Tanga</b>	<b>2,200</b>	<b>2,123</b>	<b>2,069</b>
Handeni	2,220	2,144	2,089
Kilindi	2,235	2,159	2,104
Korogwe	2,212	2,135	2,081
Lushoto	2,221	2,145	2,090
Mkinga (Maramba)	2,207	2,130	2,076
Muheza	2,205	2,128	2,074
Pangani	2,206	2,130	2,075

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
DAR ES SALAAM	2,102.12	2,071.04	1,995.40
TANGA	2,075.96	1,999.20	1,945.58
MTWARA	2,097.35	2,023.11	-

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

<b>Bandari</b>		<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
DAR ES SALAAM	Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 11.859/Tani	Ongezeko la Dola 18.720/Tani	Ongezeko la Dola 11.542/Tani
	Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 8.081/Tani	Ongezeko la Dola 11.291/Tani	Ongezeko la Dola 11.691/Tani
TANGA	Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 17.505/Tani	Punguzo la Dola 13.492/Tani	N/A
	Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 8.490/Tani	Punguzo la Dola 4.680/Tani	N/A
MTWARA	Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 17.505/Tani	Punguzo la Dola 13.393/Tani	N/A
	Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Ongezeko la Dola 8.490/Tani	Punguzo la Dola 4.680/Tani	N/A

**JEDWALI D: MWEZI HUSIKA WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA**

	<b>Aina ya Mafuta</b>	<b>Shehena ya Mafuta Ilipokelewa Mwezi:</b>	<b>Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi huu:</b>	<b>Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi uliopita:</b>
DAR ES SALAAM	Petroli	Januari 2020	Disemba 2019	Novemba 2019
	Dizeli	Januari 2020	Disemba 2019	Novemba 2019
	Mafuta ya Taa	Januari 2020	Disemba 2019	Oktoba 2019
TANGA	Petroli	Disemba 2019	Novemba 2019	Oktoba 2019
	Dizeli	Disemba 2019	Novemba 2019	Oktoba 2019
	Mafuta ya Taa	Julai 2019	Juni 2019	Juni 2019
MTWARA	Petroli	Disemba 2019	Novemba 2019	Oktoba 2019
	Dizeli	Disemba 2019	Novemba 2019	Oktoba 2019
	Mafuta ya Taa	N/A	N/A	N/A

**Nzinyangwa E. Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**